

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ofisi ya Waziri Mkuu

# Mwongozo wa kitaifa wa Kuhusisha kupunguza Unyanyapaa na Ubaguzi katika Programu za Virusi Vya UKIMWI

FEBRUARY 2009

# Contents


Utangulizi . . . . . . . . . . 1

Shukurani . . . . . . . . . . 2

Utambulisho . . . . . . . . . . 3

Dhana Muhimu . . . . . . . . . . 4

Namna ya Kukuza Kupunguza Unyanyapaa . . . . . . . . . . 6

Mwelekeo wa baadaye . . . . . . . . . . 10

Maelezo ya kuhitimisha . . . . . . . . . . 11

Kiambatanisho 1—Mfano wa machapisho ya mafunzo . . . . 12

Kiambatanisho 2—Mazoezi yanayopendekezwa katika kile kitini: *Unyanyapaa; Kitini cha Utekelezaji* . . . . . . . . . . 14

Kiambatanisho 3—Orodha ya Wakufunzi Wakuu wa Kupunguza Unyanyapaa . . . . . . . . . . 15

# Utangulizi

Shughuli za afya ya jamii zimeonyesha kwamba Unyanyapaa na Ubaguzi ni moja ya vikwazo vikubwa vya kijamii kwa majibu yanayofaa ya virusi vya UKIMWI na ugonjwa wa UKIMWI. Jamii ya kisiasa ya kimataifa ikiongozwa na shirika la umoja wa mataifa linaloshughukia UKIMWI (UNAIDS) Mwaka 2006 iliweka malengo ya upatikanaji kwa wote wa majumuisho ya miradi ya UKIMWI katika uzuiaji, tiba, uangalizi na usaidizi mpaka kufikia Mwaka 2010. Juhudi za kupunguza unyanyapaa wa UKIMWI na virusi vya UKIMWI zinaongezewa nguvu na lengo la 6 la malengo ya maendeleo ya milenia (MDGs). Nia ya lengo la 6 la malengo ya maendeleo ya milenia ni kuwa mpaka mwaka 2015 usambaaji wa virusi vya UKIMWI uwe umesimama na kupunguzwa kwa kiasi kikubwa.

Juhudi za kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI zinadhoofishwa na unyanyapaa. Kama ilivyoonekana kwenye utafiti uliofanywa na Ogden & Nyblade (2005) nchini Tanzania ambapo iligundulika kwamba unyanyapaa unaohusiana na virusi vya UKIMWI umeenea na uko katika sura tofauti. Utafiti umeonyesha pia kuwa kwa ujumla ni vigumu kwa watu wengi kutambua mitazamo na tabia zao za unyanyapaa na ni ngumu zaidi kubadilika. Kwa maana hiyo, kubadili mitazamo ya kimaadili kuna changamoto na ni suala tete.

Raisi wa Serikali ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete na mke wake mama Salma Kikwete, mwezi Julai 2007 walifanya uamuzi wa kupima virusi vya UKIMWI kwa uwazi na amekuwa akishawishi watanzania wote kutumia huduma za kupima, uangalizi na tiba zilizopo nchini. Hata hivyo, mifano mingi ya utumiaji hafifu wa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU umeelezewa kuwa unatokana na unyanyapaa unaohusiana na UKIMWI.

Tanzania inaweza kutumia harakati za kunguza ubaguzi na unyanyapaa unaotokana na UKIMWI ambazo zimekuwa zikifanyika kwa miaka kadhaa sasa li kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuboresha harakati za kupunguza unyanyapaa na ubaguzi katika miradi ya VVU na ugonjwa wa UKIMWI. Mwongozo huu uliandikwa kwa kujumuisha mafunzo bora ambayo yametokana na uzoefu wa kupunguza unyanyapaa katika mashirika kadhaa ya kijamii yanayofanya shughuli za VVU na ungonjwa wa UKIMWI. Kitini cha utekelezaji cha unyanyapaa kilikuwa muhimu katika kiuandika na matumizi ya mwongozo huu.

Japo kungeweza kuwa na miongozo inayolenga makundi tofauti, mwongozo huu ni wa jumla ambao unaweza kutumika na walengwa tofauti. Miongozo kwa walengwa maalum inaweza kuandikwa baadaye.

Juhudi za pamoja katika kupunguza unyanyapaa na ubaguzi unaohusiana na UKIMWI zinahitajika ili tuweze kutimiza lengo la 6 la Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Mwongozo huu wa kupunguza unyanyapaa ni hatua muhimu katika muelekeo huo.

**Dr. Fatma H. Mrisho**
*Mwenyekiti Mtendaji*
*Tume Ya Taifa Ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS)*

# Shukurani

Mwongozo huu wa kupunguza unyanyapaa ni matokeo ya utafiti na harakati za timu ambayo imekuwa ikihusika na harakati za kupunguza unyanyapaa kwa miaka kadhaa. Tunatambua kwa shukrani maalum msaada wa kiufundi na kipesa kutoka kwa wadau wetu wa maendeleo wa kimataifa na kitaifa. Ni vigumu kuwataja kwa majina katika ukurasa huu, lakini tunatambua mchango wao katika kazi hii.

Tume ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI inapenda pia kutanguliza shukrani za dhati kwa timu iliyoandaa mwongozo huu: Lusajo Kajula (MUHAS), Pfiriael Kiwia (KPE), Aparna Jain (ICRW), Wilbrod Manyama (KPE), Fausta Philip (MUHAS), Gideon Kwesigabo (MUHAS), Jessie Mbwambo (MUHAS), Kerry MacQuarrie (ICRW) na Laura Nyblade (ICRW) kwa kazi hii muhimu.

Tunapenda pia kutambua msaada kutoka kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, USAID kupitia FHI, Kata ya Kimara katika Manispaa ya Kinondoni, Wanajamii, Mabalozi na Kimara Peer Educators: Tatu Mustapha na Elizabeth Semwaiko. Kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi zinazohusiana na Afya cha Muhimbili (MUHAS): Dotto Elias, Rosemary Mjule, William Henerico, Francis Kassanga, Joy Maongezi, Rose Luka na Jacob Macha. ICRW: Sandra Bunch, Margo Young, Zayid Douglas, Mwelu Ndeti, Traci Eckhaus na Heidi Lary. FHI: Eric van Praag

Haitakuwa haki kumaliza bila kutaja Kikundi cha Washauri ambacho kiliwajumuisha: Dr. Gottlieb Mpangile (FHI-TUNAJALI), Dr. Eric van Praag (FHI), Jasmine Baghdellah (FHI), Prisca Kalinga (WOFATA), Feddy Mwanga (WHO), Rowland Swai (NACP), Jane Mvungi (Morogoro Regional Hospital), Moses Busiga (Pathfinder), Rev. James Chimbalambala (FBO), Mary Shuma (Futures Constella), Dr. Alban Hokororo (Balm In Gilead), Jovin Tesha (PASADA), Alex Margery (TANEPHA) , Prof. G. Kilonzo (MUHAS), Dr. Theonest Ruta (MNH), Robinah Kimbugwe (Pact Tz) na Priskilla Goba (Deloitte-TUNAJALI) kwa mchango wao wa ujuzi, uzoefu, mawazo na umakini wao kwa kazi hii.

***Kwenu wote tunasema ahsanteni sana.***

# Utambulisho

Tanzania ni nchi inayoongoza katika kujishughulisha na Unyanyapaa na ubaguzi unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI. Sera ya Taifa ya Virusi Vya UKIMWI/ UKIMWI (2001) na Sera ya Afya, Mkakati wa kitengo cha Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI (HSSP) 2008-2012 imeainisha jinsi ambavyo unyanyapaa unachangia katika ongezeko la kuenea kwa Virusi Vya UKIMWI, na kutambua kwamba kupunguza unyanyapaa ni kanuni muhimu inayohitaji kushughulikiwa na sekta zote katika ngazi zote.

Kama ilivyo katika nchi nyingi, Unyanyapaa na ubaguzi unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI upo juu sana hapa Tanzania. Katika utafiti wa hivi karibuni na watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI, asilimia 63 ya wanawake na asilimia 50 ya wanaume walitoa taarifa za kukabiliwa na unyanyapaa katika mwaka uliopita.[1] Kuanzia 2005, matunzo na matibabu bure kwa Virusi Vya UKIMWI yamekuwa fursa ya kurejesha hali ya kawaida kwa wenye Virusi Vya UKIMWI na kupunguza unyanyapaa katika nyanja ya tiba. Vikundi vya kijamii, mashirika yasiyo ya Kiserikali, watafiti, watengenezaji sera, na wadau wengine wamekuwa wakijishughulisha na unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI hapa Tanzania kuanzia janga hili lilipojitokeza. Kwa kufanya rejea katika utafiti ule wa msingi ambayo uliainisha vile vyanzo vitatu vya unyanyapaa,[2] vinavyoweza kushughulikiwa, wengi wa makundi haya wameanzisha miradi ya kupunguza unyanyapaa, kuimarisha kundi la wataalamu wa kitaifa na kuandaa vitini mahususi vya kupunguza unyanyapaa ambavyo vinapatikana katika lugha ya Kiswahili. Juhudi hizi zimeiweka Tanzania katika nafasi ya pekee katika kukuza shughuli za kupunguza unyanyapaa na ubaguzi kwenye programu za Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI.

Kwa kuendeleza juu ya misingi hii ya kupunguza unyanyapaa na ile mikakati iliyoainishwa na serikali ya Tanzania kwenye Mkakati wa kitengo cha Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI (HSSP-2008-2012), mwongozo huu umetayarishwa kutokana na uzoefu halisi ili kutoa dira kwa ajili ya programu zinazolenga kupunguza unyanyapaa. Mwongozo huu unatokana na majumuisho ya mambo tuliyojifunza, uzoefu na kazi za vitendo za vikundi mbalimbali vya kijamii katika kupunguza unyanyapaa, pamoja na kile kitini kilichofanyiwa utafiti *"Kuelewa na Kupiga vita unyanyapaa: Kitini cha Utekelezaji"* (hapa kikijulikana kama *Unyanyapaa: Kitini cha Utekelezaji*). Mwongozo huu unaainisha uzoefu wa mashirika mawili katika kutekeleza programu za kupunguza unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI kwa kutumia *Unyanyapaa:Kitini cha Utekelezaji*-Kimara Peer Educators and Health Promoters Trust (KPE) wa Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya (MUCHS).

Mwongozo huu umeandaliwa kwa matumizi ya wadau wa aina mbalimbali wanaofanya shughuli Tanzania-mashirika ya ngazi ya chini kabisa ya kijamii, watayarishaji wa mipango, wafadhili, watafiti, watunga sera, wanahabari, na watayarishaji wa mipango na watekelezaji wa shughuli za Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI katika ngazi zote- ili kuimarisha jitihada za kupunguza unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI katika nyanja zao hizo maalumu. Kwa kuanzia, mwongozo unatoa uelewa wa ujumla juu ya dhana muhimu kuhusiana na unyanyapaa na ubaguzi unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI. Kisha unafafanua kinaganaga zile ngazi tatu muhimu za kuanza kazi ya kupunguza unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI kama ifuatavyo:

I. **Anza sasa kwa kutumia rasilimali zilizopo:** Rasilimali; watu wenye ujuzi na vitini vya kupunguza unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI vipo Tanzania na vinapatikana.

II. **Unganisha** shughuli na ujumbe wa kupunguza unyanyapaa katika programu zilizopo za Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI.

III. **Washirikishe wadau muhimu** ili kupanua wigo wa matokeo.

Hatimaye, mwongozo unajumuisha kwa mapendekezo ya jinsi ya kukuza shughuli za kuunganisha upunguzaji wa unyanyapaa nchini.

# Dhana Muhimu

Kabla ya kuelezea kwa ukamilifu zile njia tatu za kupunguza unyanyapaa katika programu za Virusi Vya UKIMWI, mwongozo huu unatoa mwanga juu ya dhana muhimu kuhusiana na unyanyapaa na ubaguzi.

## Unyanyapaa ni Nini?

" Unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI unaweza kuelezewa kama ni "mchakato wa kupunguza thamani" ya mtu ama akiwa anaishi na Virusi Vya UKIMWI ama anahusiana na Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI. Unyanyapaa huu mara nyingi unaanzia katika misingi ya unyanyapaa kwenye ngono na utumiaji wa dawa za kulevya kwa kujidunga sindano—ambazo ni njia kuu mbili kuu za kupata Virusi Vya UKIMWI. Ubaguzi hufuatia baada ya unyanyapaa na ni kutendewa visivyo sawa na kwa isivyostahili kwa mtu kutokana na hali halisi ama ya kudhaniwa juu ya hali yake ya uambukizo wa Virusi Vya UKIMWI. Ubaguzi unatokea wakati ambapo utofautishaji unafanyika dhidi ya mtu unaopelekea kutendewa visivyo sawa na isivyostahili kwa misingi ya kuwa miongoni au kuhisiwa kuwa miongoni mwa kundi Fulani." (UNAIDS:Jarida la maelezo halisi ya unyanyapaa na ubaguzi, Desemba 2003, www.unaids.org)

## Unyanyapaa unafananaje?

Unyanyapaa na ubaguzi (unaoelezewa kama vitendo vinavyochukuliwa na watu ama taasisi kutokana na unyanyapaa) unaweza kujitokeza katika mlolongo wa manma nyingi zikiwemo: za kutengwa na kutoshirikishwa kijamii (m.f. kutengewa vyombo vya chakula, kutengwa wakati wa matukio ya kijamii) ikijumuisha kufanyiwa vurugu, maneno (m.f. kutetwa, kupachikwa majina ama kunyooshewa vidole); kupoteza utambulisho na hadhi (m.f. kupoteza heshima katika familia na jamii); na taasisi (m.f. kufukuzwa kazi, nyumba au wateja). Unyanyapaa unaweza pia kuwepo kwa ndani na kuathiri jinsi watu wanavyofikiria juu yao wenyewe. Kwa mfano watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI wanaweza kujiwekea kwa ndani unyanyapaa unaowakabili na kusababisha wajionee aibu, hawana hadhi, kudhalilika ama kukosa maana. Hii inaweza kuwazuia kutafuta huduma za matunzo ama tiba ama kuchukua fursa za maisha kama vile kuendeleza elimu, kupanda cheo au kuanzisha biashara.

## Ni nini kinasababisha unyanyapaa na ni kwa namna gani unaweza kushughulikiwa?

Mwaka 2005, utafiti linganishi uliofanyika Ethiopia, Tanzania, Vietnam na Zambia ulibainisha kwamba unyanyapaa upo dhahiri kote kwa mfumo wa aina, matokeo na vyanzo vikuu[4,5] Tafiti hizi ziliainisha vyanzo vikuu vitatu vya unyanyapaa vinavyoweza kushughulikiwa: (1) Utambuzi mdogo wa unyanyapaa; (2) Hofu ya kuambukizwa Virusi Vya UKIMWI kwa kugusana; na (3) Kuthaminisha watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kwa kuhusisha kuwa walitenda kinyume na maadili.

### Utambuzi mdogo wa Unyanyapaa

**Sababu:** Mara nyingi watu hawatambui kuwa mitizamo yao, maneno na matendo yananyanyapaa watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI na yanasababisha athari mbaya. Utafiti uligundua kwamba hata wale wenye nia njema kwa watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI mara nyingine wanawanyanyapaa bila kutambua.

**Pendekezo la kiutendaji:** Kuongeza uelewa kuhusu unyanyapaa ni nini na madhara yake kwa watu, familia na jamii ni hatua muhimu ya awali katika kupunguza unyanyapaa. Programu zinaweza kuanzisha uhamasishaji katika njia nyingi ikijumuisha kupitia kwenye kuandaa machapisho ya taarifa, elimu na mawasiliano ambayo yatatoa taarifa kuhusu unyanyapaa unaohusishwa na VIrusi Vya UKIMWI na muonekano wake, na matukio yanayowafikia jamii kule waliko.

## Hofu ya kuambukizwa Virusi Vya UKIMWI kwa kugusana (Unyanyapaa unaotokana na hofu);

**Sababu:** Hofu kwamba Virusi Vya UKIMWI vinaweza kuambukizwa kwa kugusana, kwa mfano kupitia njia zisizo za kuingiliana kama vile kumgusa mtu anayeishi na Virusi Vya UKIMWI au kushirikiana sahani za chakula na vyombo, vinaleta unyanyapaa wa mfumo wa kutenga. Hofu hizi za kila siku zisizo na misingi, utaratibu wa mahusiano ya kawaida vinasababisha watu kubadili tabia zao na kuwakwepa watu wanaoishi na VIrusi Vya UKIMWI.

**Pendekezo la kiutendaji:** Kudumisha na kuendelea kutoa taarifa sahihi kuhusu uambukizo wa Virusi Vya UKIMWI kunahitajika ili kupiga vita hofu zisizo za msingi za uambukizo kutokana na mahusiano ya kawaida. Programu zinaweza kushughulikia hofu hizi kupitia maonyesho katika radio za kwenye jamii zao, maonyesho kwenye jamii, mfumo wa waelimishaji rika na vijarida.

## Kuwathaminisha watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kwa kuhusisha kuwa walitenda kinyume na maadili.

**Sababu:** Thamani zinazoongozwa na taratibu za kijamii, jinsia na kanuni zinazohusu ngono mara nyingi zinahusisha watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kuwa wametenda kinyume na "maadili." Kwa mfano, mara nyingi dhana zinajengeka kwamba watu wanaoishi na VIrusi Vya UKIMWI walipata uambukizo kutokana na tabia inayoaminika kijamii kuwa kinyume na "maadili" na "zisizokubalika" kama vile kutokuwa mwaminifu au mfuska, huelekeza aibu na lawama kwa watu wanaoishi na Virusi VYa UKIMWI, na mara nyingine kwa familia zao pia.

**Pendekezo la kiutendaji:** Kuchochea kuwepo kwa uwazi na mazungumzo elekevu kuhusiana na mahusiano ya ngono, hisia na mazingira ambamo tabia hatarishi zinatokea. Programu zenye mafanikio katika kupunguza unyanyapaa zinampa kila mtu na taasisi muda wa kutosha na mianya ya kujitafakari na kubadilika. Unyanyapaa umejikita sana na kuwa na mwelekeo wa kutofautiana kati ya mtu mmoja na mwingine. Watu wanahitaji muda wa kutosha na nafasi kuchunguza mitizamo yao na tabia kabla hawajawa na ari na msimamo wa kubadilika.

# Namna ya Kukuza Kupunguza Unyanyapaa

## I. Anza sasa kwa kutumia rasilimali zilizopo

Tanzania ina vifaa mahsusi, vilivyofanyiwa majaribio na vilivyopo katika lugha ya Kiswahili ambavyo vinaweza kutumiwa na makundi-lengwa mbalimbali; kundi la wakufunzi ambao wapo tayari kuwashirikisha wengine ujuzi na uzoefu wao na machapisho yanayopatikana kwa ajili ya kutumika kwa kazi hii (Kiambatanisho 1). Muhimu zaidi, unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI ni suala la kijamii hivyo kila mtu anao wajibu wa kulishughulikia.

### Rasilimali # 1: Unyanyapaa: Kitini Cha Utekelezaji.

Kitini cha utekelezaji kinatoa mkusanyiko wa mazoezi shirikishi na ya kutumia ili kuongeza ufahamu na kuhamashisha kushughulikia na kuchochea vitendo dhidi ya unyanyapaa. Kinatoa mianya kwa jamii mbalimbali na makundi-lengwa kutambua unyanyapaa ni nini na una sura gani, kuelewa vyanzo vyake na athari zake, na kupanga mikakati ya kukabiliana nao. Mazoezi haya yameandaliwa kutokana na mchakato shirikishi wa kujifunza, kushirikishana hisia na uzoefu, kuchambua mambo na kuchukua hatua. Mazoezi yanayopendekezwa yamejumuishwa katika Kiambatanisho 2.

Kitini hiki, ambacho kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, kinajumuisha sura mbalimbali zinazoshughulikia unyanyapaa katika mazingira mengi mbalimbali. Kimetumika sehemu nyingi hapa Tanzania na wanajamii wa aina tofautitofauti wakiwemo wahudumu wa afya, watoa huduma majumbani, vijana, viongozi wa dini, viongozi wa kijamii, watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI, watendaji wa asasi zisizo za kiserikali na za kijamii. Uzoefu wa programu umeonyesha kwamba kitini kinatoa lugha muafaka ya kuwasiliana juu ya mambo magumu miongoni mwa makundi mbalimbali, hasa katika masuala magumu kama ngono. Kwa mfano, zoezi la *"Kuvunja ukimya kuhusu ngono,"* linafanya kazi vizuri sana wa kuwapatia viongozi wa dini njia ya kujadili changamoto zilizopo kwenye masuala haya. Kitini pia kinatoa lugha iliozoeleka na kauli rahisi kwa watu wanaotoka katika uzoefu na taswira tofauti tofauti kuzungumza pamoja kuhusu unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI. Hii lugha iliozoeleka inawezesha pawepo mjadala ambao unakuza uelewa na kukubaliana.

### Rasilimali # 2:Wakufunzi wakuu

Kundi la wakufunzi wakuu wa kupiga vita unyanyapaa wapo sehemu zote hapa Tanzania (Tazama kiambatanisho 3). Wanapatikana na wanaweza kutumika na yeyote anayehitaji msaada wa kitaaluma katika programu za kupunguza unyanyapaa na kutoa mafunzo kwa wengine katika kupunguza unyanyapaa.

### Rasilimali # 3: Machapisho ya Taarifa, Elimu na Mawasiliano.

KPE na TUMAINI program wameandaa vijarida rahisi-rafiki vya taarifa, elimu na mawasiliano. Vimeandaliwa ili kuelezea unyanyapaa kwa lugha rahisi, na vinatumia michoro rahisi (tazama kiambatanisho 1) kuelewa ujumbe. Vijarida hivi vimesambazwa wakati wa mikutano inayowafikia watu kule walipo, wakati wa huduma za majumbani na katika sehemu za huduma za afya na vimepokelewa vizuri sana na wanajamii.

## II. Husisha shughuli na ujumbe wa kupunguza unyanyapaa katika programu zilizopo za Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI ili kuhakikisha uendelevu.

Asasi zinazofanya kazi za kuzuia maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI, matunzo, tiba na msaada zinahitajika kuhusisha programu za kupunguza unyanyapaa na ubaguzi katika shughuli zilizopo ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu unakuwepo. Kwa kutumia mtizamo huu wa kuhusisha, hapatahitajika mfumo mpya wa kuhimili shughuli na huduma. Kwa hali hiyo, hapatakuwepo uhitaji

wa kutenga fedha zilizopo kwa ajili ya mpango wa pekee wa unyanyapaa na ubaguzi badala ya zile zinazotengwa kuanzisha shughuli ya kuhusisha. Hii haina maana kusema kwamba kuhusisha ndiyo njia pekee ya kufuata—kuongezea shughuli maalumu za unyanyapaa na ubaguzi kwenye mradi inawezekana pia na mara nyingi hii ndio muafaka na inakubalika. Shughuli mahsusi zinazolenga kupunguza unyanyapaa zinaweza kuwa na nafasi nzuri katika mazingira maalumu kama vile kampeini za kupunguza unyanyapaa kwa vijana, watoto yatima na walio hatarini, na katika vituo vya huduma za Afya, n.k.

Kuhusisha kupunguza unyanyapaa katika programu za Virusi Vya UKIMWI zinazoendelea inahusisha hatua tano: (1) Tathmini uwezo wa taasisi zilizopo; (2) Shughulikia unyanyapaa ndani ya asasi itakayohusika; (3) Tathmini walengwa; (4) Panga na anzisha kuunganisha; na (5) Fuatilia na fanya tathmini ya juhudi zilizofanyika. Hatua ya kwanza hadi ya tatu, ambazo zinahusu tathmini halisi ya taasisi, zaweza kuchukua muda wa siku mbili hadi majuma mawili kutegemeana na ukubwa wa taasisi na kundi lengwa.

## Hatua ya 1: Tathmini uwezo wa taasisi.

Ili kung'amua njia nzuri ya kuhusisha shughuli za kupunguza unyanyapaa katika mradi unaoendelea, inahitajika kufanya tathmini ya taasisi na uhimili wa bajeti, sera, taratibu, uwezo, mianya na mahitaji ya watendaji.

## Hatua ya 2: Shughulikia unyanyapaa ndani ya asasi itakayohusika.

Programu za kupunguza unyanyapaa zenye mafaniko hutoa nafasi ya kutosha kwa kila mtu na taasisi, fursa na msaada wa kujifunza, kujichunguza na kupata uelewa na stadi muhimu za kubadilika. Hata kama watendaji wamekuwa wakifanya kazi ya kuzuia maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI, matunzo ama tiba kwa muda mrefu, wanaweza kuwa na mambo, hofu na uelewa potofu ambapo hawajawahi kujisikia huru kupata ufafanuzi juu yake. Kwa mfano; japokuwa watendaji wa KPE walikuwa na uelewa juu ya jinsi Virusi Vya UKIMWI vinavyoambuizwa, watendaji wengine walielezea hofu ya kuambukizwa Virusi Vya UKIMWI wanapokwenda nyumbani kwa mtu anayeishi na Virusi Vya UKIMWI. Watendaji wengine walikiri kwamba hata wanapogundua kwamba mtu fulani anaishi na Virusi Vya UKIMWI, wanaamini kwamba mtu huyo atakufa angali kijana ingawaje wanajua ukweli kuhusu "Dawa za Kupunguza makali ya VIrusi VYa UKIMWI (ARVs) na kuimarisha afya bora. Wao, pamoja na watu wengine wengi, walikuwa bado hawajatafakari kwa undani kwamba watu wenye kuishi na Virusi Vya UKIMWI wanaweza kuishi kwa muda mrefu na afya njema.

## Namna ya kushughulikia unyanyapaa ndani ya taasisi yako.

Tumia kile kitini: *Unyanyapaa:Kitini cha Utekelezaji* kufunza watendaji wote. Kwa kutegemeana na matokeo ya tathmini, malengo na shughuli ya mafunzo iliyopangwa, kitini kitatoa fursa ya mabadiliko katika muda na kiwango cha mafunzo. Kitini kinatoa ile fursa ya kujifunza na kujichunguza na kugundua hofu zisizoongelewa na imani ambazo kwa bahati mbaya zinapelekea katika mitizamo na tabia za kunyanyapaa na pia njia za kuhusisha ujumbe wa kupunguza unyanyapaa katika kazi inayoendelea.

Namna nyingine ni kutuma watendaji wachache kwenye mafunzo ya wawezeshaji. Kisha hawa watendaji waliopata mafunzo wanaweza kuendesha mafunzo katika taasisi yako kwa wale watendaji wengine waliobaki. Wale watendaji waliopata mafunzo wanaweza pia kuisaidia taasisi kufikiria namna muafaka katika kuhusisha.

Kwa hali hiyo, kabla ya kuanza kufanya kazi na wanajamii na watu wengine nje ya taasisi ama mradi wako, ni muhimu kutoa mianya kwa watendaji kujichunguza na kutambua unyanyapaa katika kazi zao na maisha yao wenyewe. Kile kitini *Unyanyapaa:Kitini cha Utekelezaji* kinaweza kutumika kutekeleza hili katika njia salama na isiyo ya kutisha, kuwaongezea watendaji umahiri kwa wegine na ukweli kwa mamna wanavyowasaidia na kuwatunza watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI na familia zao.

## Hatua ya 3: Tathmini walengwa.

Kutathimini walengwa kutatoa fursa ya kuelewa hali halisi ya unyanyapaa na ubaguzi iliyopo katika kundi hilo (m.f. jamii, huduma za afya, wanahabari, n.k.) Taarifa zilizokusanywa zitatoa mwelekeo wa kuandaa aina ya programu inayostahiki.

Tathmini ya walengwa inaweza kujumuisha:

- Majadiliano ya vikundi na watendaji au wanajamii au viongozi.
- Zoezi la kuainisha maeneo ili kutambua unyanyapaa unatokea wapi katika jamii ile, au kuchambua kwa kina vyanzo vya unyanyapaa.

### Hatua ya 4: Panga na anzisha kuunganisha.

Mara unapokamilisha tahmini (yaani; hatua 1-3 hapo juu), taasisi itakuwa imejiweka katika nafasi nzuri kuanza mchakato wa kuunganisha unyanyapaa katika programu. Mifano ifuatayo hapa chini inaonyesha mchakakato na matokeo ya hayo katika taasisi tatu tofauti.

### Hatua ya 5: Fuatilia na fanya tathmini ya juhudi zilizofanyika.

Hatimaye, kama ilivyo kawaida katika programu yoyote, ni muhimu kusimamia na kutathmini matokeo ya kuhusisha kupunguza unyanyapaa na ubaguzi katika shughuli. Ufuatiliaji ni lazima ushirikishe na uelewa wa jamii katika kushughulikia unyanyapaa. Viashiria muafaka vya kupimia vinapatikana kwa ajili ya kupima mabadiliko ya unyanyapaa na ubaguzi miongoni mwa walengwa mbalimbali, ikijumuisha jamii, watoa huduma za afya na watu wanaoishi na Virusi VYa UKIMWI.[6]

## III.Washirikishe wadau muhimu ili kupanua wigo wa matokeo.

Pamoja na kuhusisha kupunguza unyanyapaa katika programu zote zinazoendelea, kupungua kwa unyanyapaa kunaweza kuimarishwa kwa kuwashirikisha wabia wakuu wawili: (1) Viongozi wenye ushawishi mkubwa katika jamii; (2). Watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI. Ile tathmini halisi inaweza kusaidia kuainisha mianya ya kufanikisha hili.

### Shirikisha Viongozi Muhimu.

Eneo muhimu la nyongeza katika programu za kupunguza unyanyapaa ni kwa kufanya kazi na viongozi muhimu tangu awali ili kupanua na kuchochea upunguzaji wa unyanyapaa. Ingawa kubadili tabia huanzia kwa mtu binafsi, ili badiliko hilo liwe la kudumu, taratibu za kijamii ambazo zinatoa msukumo na kuimarisha kuwepo kwa unyanyapaa ni lazima pia vibadilike. Uzoefu umeonyesha

## Taasisi tatu waoliohusisha kupunguza Unyanyapaa na Ubaguzi katika programu zao zinazoendelea

***Mfano 1.*** KPE waliunganisha ujumbe wa unyanyapaa na ubaguzi katika shughuli zao zinazoendelea za “kuburudisha na kufundisha” jamii kwa kuandaa maigizo, hadithi-vichekesho na nyimbo zikilenga unyanyapaa na ubaguzi. Walitumia pia mazoezi shirikishi mbalimbali na zana kutoka katika kile kitini *Unyanyapaa:Kitini cha Utekelezaji* katika majadiliano na wanajamii baada ya kipindi cha burudani. Zaidi ya hayo, KPE waliongezea shughuli mahususi za unyanyapaa na ubaguzi katika mpango wao wa kazi, kama vile kuwafikia Mabalozi ambao ni viongozi wa kijamii hapa Tanzania. Hii ilijumuisha kuwafundisha katika warsha juu ya vyanzo vya kawaida na athari za unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI kwa kutumia kile kitini- *Unyanyapaa:Kitini cha Utekelezaji* na kisha kuwapatia msaada wa kitaaluma wa jinsi ya kuhusisha programu za unyanyapaa na ubaguzi katika wajibu wao unaoendelea.

***Mfano 2.*** Tathmini halisi ya taasisi ya Students Partnership Worldwide (SPW) ilisaida katika kuhusisha shughuli za kupunguza unyanyapaa na ubaguzi sio tu kwa walengwa wake, bali pia miongoni mwa watendaji wake. SPW ambao wanatoa elumu ya afya ya uzazi kwa vijana ndani na nje ya shule, waliandaa na kutekeleza programu ya mafunzo ya wakufunzi juu ya kukuza uelewa na kupunguza unyanyapaa kwa watendaji wake kwa msaada wa wakufunzi kutoka KPE na MUHAS. Baada ya mafunzo, SPW waliandaa programu ya radio iliyoitwa “positive voice” (Sauti Chanya) iliyolenga kuwasaidia vijana kuelewa na kushughulikia kwa pamoja unyanyapaa wa hofu na msukumo wa kijamii na pia jinsi ambavyo unyanyapaa unaweza kuathiri vibaya uwajibikaji katika tabia ya ngono, mfano kwa kuwakatisha tamaa wale ambao tayari wanao ama wanahofiwa kuwa na uambukizo wa Virusi Vya UKIMWI, kuacha kupata huduma ya kupima, matunzo na huduma za tiba.

***Mfano 3.*** Kutoka 2004-2006, mradi wa TUMAINI (ukifuatiwa na FHI/Deloitte mradi wa TUNAJALI mwaka 2007) walihusisha shughuli za unyanyapaa na ubaguzi katika programu za huduma majumbani kwa watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kwa kuwapa mafunzo watekelezaji wote wale watendaji wa kujitolea ili wang’amue na kuutambua unyanyapaa na athari zake na pia kuandaa hatua za utekelezaji za kushughuklikia unyanyapaa kama watoa huduma na katika nyumba wanazozifikia. Mafunzo ya wakufunzi yalifanyika kwa watekelezaji wakuu ili nao waweze kutoa mafunzo kwa watendaji wapya na wale wa kujitolea kama watatokea kubadilishwa.

## Uzoefu wa KPE katika kuwashirikisha viongozi muhimu

KPE waliwashirikisha Mabalozi katika programu ya unyanyapaa na ubaguzi tangu awali kabisa. Mabalozi walishiriki pamoja na watendaji wa KPE katika mafunzo ya wawezeshaji, ili kuwapa fursa ya kutafakari unyanyapaa ndani mwao na katika maisha yao, pamoja na kujifunza stadi za uwezeshaji katika kutoa ujumbe na kuchukua hatua juu ya unyanyapaa na ubaguzi. Mabalozi walikuwa rasilimali muhimu katika jamii zao, walitoa rufaa na msaada kwa watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI, na walishawishi kwa niaba ya watu wanaoishi na VIrusi Vya UKIMWI ambao walikabiliwa na unyanyapaa. Kwa mfano, Balozi mmoja alimsaidia mtoto mmoja yatima ambaye wazazi wake walikuwa wamefariki kutokana na UKIMWI. Ndugu walikuwa wamenyang'anya nyumba ya familia ya mtoto yule yatima. Yule Balozi alipeleka kesi ile katika mahakama ya mwanzo na kufanikiwa kutetea. Ile mali ilirudishwa kwa yule mtoto. Uzoefu wa KPE umeonyesha pia kwamba jamii wanawaona Mabalozi kuwa wanawajibika kuimarisha taratibu mpya za kijamii kupinga vitendo vya unyanyapaa. Kwa mfano, wanajamii walimuwajibisha Balozi kulinda haki za mali za watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, hasa wanawake na watoto walioathirika na VIrusi Vya UKIMWI na UKIMWI, kwa sababu walijua kwamba Mabalozi walikwisha kujifunza ni kwa jinsi gani kunyang'anya mali kunaweza kuwa aina moja mbaya ya unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya UKIMWI.

kwamba viongozi mashuhuri ndani ya jamii wanakuwa mfano wa tabia na wanaweza kuwa kigezo cha kuanzisha taratibu mpya zisizo na kunyanyapaa, ambazo zitachochea badiliko katika jamii. Kwa kuwatumia watu sahihi, programu inaweza kuimarisha mtandao wa wanaharakati wa kupinga unyanyapaa (mawakala wa mabadiliko) watakaoongoza kwa mfano na kuwa kigezo cha kuigwa kwa tabia inayokubalika.

## Ushirikishwaji mahiri wa watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI

